



**NOTISI KWA WAAJIRI KUWASILISHA TAARIFA YA MAPATO YA MWAKA YA
WAFANYAKAZI KATIKA MFUKO WA FIDIA KWA WAFANYAKAZI**

Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidial kwa Wafanyakazi (WCF) anawataarifu waajiri wote Tanzania Bara kuwasilisha taarifa ya mapato ya wafanyakazi wao (Return of Annual Earnings) kwa kipindi cha mwaka mmoja, yaani kuanzia tarehe **01.03.2019 mpaka tarehe 28.02.2020**.

Uwasilishwaji wa taarifa hizo ni kwa mujibu wa Kifungu cha 73 (1) na (2) cha Sheria ya Fidial kwa Wafanyakazi [Sura ya 263 Marejeo ya Mwaka 2015] kinachotaka kila mwajiri kuwasilisha taarifa hizo kila mwaka kabla ya tarehe 31 Machi.

Kwa tangazo hili, nawataarifu waajiri wote kuwa uwasilishwaji wa taarifa hizo ni kwa kutumia fomu **WCR – 3** kwa njia ya mtandao wa kielektroniki (**Employers' Online Self-Service Portal**) unaopatikana katika kiunga cha tovuti <https://portal.wcf.go.tz> na mwisho wa kuziwasilisha ni **tarehe 31.03.2020**.

Kwa waajiri ambao hawajaanza kutumia huduma za mtandao, fomu zilizojazwa kikamilifu ziwasilishwe kwenye ofisi za Mfuko zilizopo ghorofa ya 6, Jengo la GEPF House, Kitalu na 37, Regent Estate, Barabara ya Bagamoyo au ofisi za Mfuko za mikoani au Ofisi za Kazi zilizopo mikoani na wilayani Tanzania Bara.

Aidha, fomu WCR - 3 inapatikana kwenye tovuti ya Mfuko www.wcf.go.tz, Makao Makuu ya Mfuko au kwenye ofisi za Mfuko za mikoani au ofisi za Kazi zilizopo mikoani na wilayani Tanzania Bara.

Kwa mawasiliano Zaidi piga simu bure 0800110028 au 0800110029.

Imetolewa na:

Idara ya Uhusiano

Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF)

Kitalu na. 37, GEPF House, Barabara ya Bagamoyo, Regent Estate, Ghorofa ya 6.

S.L.P 79655,

Simu: +255 22 2926107, +255 22 2926108,

Nukushi: +255 22 2926109, Barua pepe: info@wcf.go.tz,

Tovuti: www.wcf.go.tz,

DAR ES SALAAM.